# MIUJIZA

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha  MIUJIZA. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MIUJIZA

1.Miujiza?…………………………………………………………..

2. Kusudi la Miujiza ……………………………………………..

3. Karama ya miujiza…………………………………………….

4. Maombi……………………………………………………………

5. Wokovu…………………………………………………………...

6. Yesu ni Mtenda miujiza……………………………………..

9.Kuokoka………………………………………………………….

10. Mwisho…………………………………………………………

a

# 1. MIUJIZA?

Miujiza ni matendo mema makuu na ya  ajabu ya mungu huwatendea wanadamu wamwaminio kwa moyo anaweza kutenda au kufanya au hutenda machoni pa wanadamu kuwastajabisha na kudhirisha nguvu zake ili jina lake lituzwe yaani jina la Yesu.

Miujiza ni hatua ya mwisho mungu kujionyesha kwa wazi machonoi pa wanadamu wenye dhambi na wenye haki,waliokoka na wasiokoka.

Miujiza tunaweza kuiweka  ktk sehemu kuu mbili  nazo ni zifuatazo:

**1) .Miujiza ktk mwili wa mtu**

Mfano wa miujiza ktk mwili wa mtu ,miujiza ya kurejeshewa kiungo kipya ulichopoteza kama titi,mguu,pina,vidole,figo, na ile ya ufufuko wa mtu kabla hajazikwa au amezikwa ana siku nne  au amebaki mifupa., Bikira mariamu akupata mimba na kumzaa Yesu kwa uweza wa Roho mtakatifu.

**2). Miujiza ktk vitu alivyoumba mungu au walivyotengeneza wadamu**

Mfano wa miujiza ktk  vitu alivyoumba mungu au walivyotengeneza wadamu  kuna maji kuwa divai, samaki na mikate michache kubarikiwa na yesu kulishwa zaidi ya watu elfu tano,Yesu kutembea juu ya bahari,Yesu kukausha mtini,Yesu  kubariki petro kwa kuvua samaki wengi mahali ambapo hakupata usiku kucha,nabii musa mungu kupasua bahari na kufanya njia,maji ya mto kuwa damu,nabii eliya moto kutoka mbinguni kushuka na kutekweza sadaka,kuni na maji,kulishwa mkate na kunguru siku tatu, kula na mjane mwezi mtu,nabii Elisha kulipia deni mama aliyedaiwa kwa kiasi kidogo cha mafuta kilichojaza na madumu kadhaa yasiyo na maffuta kisha mama kwenda kuuza na kulipa deni.

Mifano hiyo unaweza kuipata ktk biblia msome Yesu, Musa & Eliya.

## 2.KUSUDI LA MIUJIZA

Kusudi l a miujiza au kazi ya miujiza aitendayo mtu kwa watu au kwa kanisa yaani waliokolewa kutoka ktk maisha ya dhambi na mungu au wakristu waliokoka.

1) Miujiza ipo kwa ajili ya wasioamini habari za yesu mfufuka wenye dhambi kupitia hiyo wapate kukutana mungu na kumwamini Yesu na kuokoka kisha kumfuata kumtii kama bwana na mfalme.
2) Miujiza ipo kwa ajili ya waaminio au wakristu waliokoka wenye mashaka kama tomaso mtume wengine wametembea ktk wokovu lakini kuna mambo wanayatilia mashaka miujizaipo ili kuwaondolea mashaka yao ili wasiingie hukimu.

**Yohona 20.24**

" ...Basi, baada ya siku nane, wanafunzi wake walikuwamo ndani tena, na Tomaso pamoja nao. Akaja Yesu, na milango imefungwa, akasimama katikati, akasema, Amani iwe kwenu.

Kisha akamwambia Tomaso, Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu, wala **usiwe asiyeamini, bali aaminiye.** "

3)Miujiza ipo ili kukupa hekima uliyeokoka au mtumishi wa Yesu kwa kuitafakari ukiongozwa na Roho mtakatifu ili kuilisha Roho yako.Hivyo hekima iliyomo ktk miujiza ya mungu inapatikana kwa kuitafakari.

**Zaburi 119: 7**

"Sheria ya Bwana ni kamilifu, Huiburudisha nafsi. **Ushuhuda wa Bwana** ni amini, Humtia mjinga **hekima.** "

4) Miujiza ipo ili jina la Yesu litukuzwe. **Mathayo 6:9**

"Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, **Jina lako litukuzwe, Ufalme** wako uje,"

# 3. KARAMA YA MIUJIZA

Miujiza ni karama ambayo roho mtakatifu hugawia wakristo waliokoka na kujazwa nguvu zake wale aliokusudia kuwa watumishi wa Yesu au Baba yake.

Ktk kanisa karama ya miujiza ni roho mtakatatifu huweza kuwapa manabii,mitume,wahubiri ,wainjilisti na watenda miujiza yaani watumishi wenye huduma ya miujiza.

Mfano wa manabii waliopewa karama ya miujiza waliomo ktk kitabu cha biblia  manabii Musa, Eliya na Elisha.

Mfano wa mitume  waliopewa karama ya miujiza waliomo ktk kitabu cha biblia  mitume Petro na Paulo.Mojawapo ya muujiza ni ule wa kufufua (dorkasi na mtu aliyeanguka na kulala kama kafa kutoka ghorofa ya mitume)

**Matendo ya mitume 9: 36 – 40**

"Na mwanafunzi mmoja alikuwako Yafa, jina lake Tabitha, tafsiri yake ni Dorkasi (yaani paa); mwanamke huyu alikuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa.  Ikawa siku zile akaugua, akafa; hata walipokwisha kumwosha, wakamweka orofani.  Na kwa kuwa mji wa Lida ulikuwa karibu na Yafa, nao wanafunzi wamesikia ya kwamba Petro yuko huko, wakatuma watu wawili kwake, kumsihi na kusema, Usikawie kuja kwetu.  Petro akaondoka akafuatana nao. Alipofika, wakampeleka juu orofani wajane wote wakasimama karibu naye, wakilia na kumwonyesha zile kanzu na nguo alizozishona Dorkasi wakati ule alipokuwa pamoja nao.  Petro akawatoa nje wote, akapiga magoti, akaomba, kisha akaelekea yule maiti, akanena, Tabitha, ondoka. Naye akafumbua macho yake, na alipomwona Petro akajiinua, akaketi. "

Mfano wa wahubiri  waliopewa karama ya miujiza waliomo ktk kitabu cha biblia  mhubiri filipo moja wa  muujiza ni ule wa kunyakuliwa toka kwa towasha wa kushi baada ya kumbatiza hadi Azoto.

# 4. MAOMBI

Maombi ya mtumishi wa Mungu mwenye karama au huduma ya miujiza ni yafuatayo;=>

1) Kuombea wale wanaotendewa miujiza na wenye dhambi waokoke.
2) Kuombea wasioamini na wenye dhambi waonapo miujiza wakutane na neema ya mungu kuamini na kuokoka.
3) Kuombea wale wenye mashaka waaminio na waliokoka waonapo miujiza ya mungu waondolewe mashaka yao na hukumu pia.
4) Kuwaombea waaminio na wasioamini waonapo miujiza walitukuze jina la Bwana Yesu na Baba yake.
5) Kuwaombea wale waonaomiujiza ya mungu wawashudie au kuwahubiri wengine wasiona au wayasimulie kwa uzao wao yaani vizazi hata vizazi.
6) Mungu ni mtakatifu sehemu kubwa ya miujiza hutendwa na mungu wa Israeli mwombe mungu siku zote akupe kutembea ktk utakatifu wa miujiza yake.
7) Kuombea wale waonao miujiza ya mungu wenye kuamini na waliokoka wapate hekima kwa kutafakari miujiza itakayosaidia kutatua changamoto wanazokutana nazo na kuwapa ufahamu na maarifa ya mungu yaani baba yake Yesu . Kukua ktk kujua uweza wa mungu au nguvu zake.
8) Maombi ya kumshukuru na kusifu Mungu kila akutumiapo kutenda miujiza Kama wewe ni mtumishi wa Yesu mwenye karama au huduma ya miujiza ya Mungu.
9) Maombi ya kuomba roho mtakatifu akuongoze ktk kweli uwe huru ktk wokovu wako usitende dhambi.

# 4.WOKOVU

.**Wokovu** ni maisha ya mtu aliyeokoka kama matokeo ya kutendewa mema na mungu mfano miujiza,uponyaji,kutolewa pepo au kufunguliwa,kubarikiwa,kutajirishwa,kupewa ulinzi wa malaika , kujazwa furaha,Amani,Haki and Upendo.

Wokovu kwa waliokoka uletwa kwao na kudhihirika ktk maisha ya kila siku kutokana yupo chini ya huduma ipi ya kanisa pia na huduma iliyo ndani yako au karama unapochochea au kuitumia kupenda kanisa kama Yesu alivyoamuru yaani kuitumia kuhudumia wenzako waliokoka.

Wokovu wa Mtumishi wa Yesu mwenye huduma ya miujiza au karama ya miujiza maisha yake yanakiwa kujaa miujiza ya mungu uchumi wake ni kimiujiza, ndoa kimiujiza, tabia za kale zibadilishwe kimiujiza. Ili kutunza huduma yake na Karama ya miujiza Yafuatayo ni baadhi ya mambo ya kuzingatia :

1) Uwe mwenye tabia ya imani na mwenye kumwamini mungu ktk mambo madogo hadi makubwa yasiyowezekana kuwa yanawezekana kwake.
2) Kuombea miujiza waliokoka au wasiokoka waliopewa neema ya mungu kuamini uweza wa mungu.
3) Kuombea miujiza waliokoka wenye mashaka waliopo kanisani siku ya sabato au siku saba ya kukusanyika watakatifu ,wakristo au waliokoka kwa ajili ya Bwana Yesu mfano Jumapili kuwaondolea mashaka.
4) Roho Mtakatifu akuongoze ktk kweli ufikie utukufu wa kushudiwa na watu una dhambi na roho mtakatifu ndani yako maisha yako ya wokovu huna dhambi mbele za mungu na yesu amekuweka huru kutoka ktk utumwa na dhambi umekuwa mwana wa Mungu kama

## 5. YESU NI MTENDA MIUJIZA

Kweli Yesu ni mtenda miujiza yeye ni kwanza wa watumishi wa Mungu wenye karama au huduma ya miujiza. Baadhi ya miujiza ya Yesu ni:

1) Kuzaliwa kwa Yesu bikira mariamu kwa uweza wa Roho mtakatifu.
2) Roho mtakatifu kushuka juu ya Yesu baada kubatizwa na Yohana mbatizaji kwa wa hua (njiwa dume)
3) Maji kuwa divai na Kutembea juu ya bahari.
4) Samaki na mikate michache kulishwa kwa watu elfu tano
5) Kutiisha upepo na mawimbi makubwa bahari
6) Kumpatia shekeli ya kulipia kodi Petro kwa kumwagiza akavue samaki na samaki wa kwanza kumvua ampasua itaikuta shekeli akalipe kodi kwa ajili yake na petro.
7) Kumfufua Lazaro ,kijana alikufa alikuwa anaenda kuzikwa wa mjane na mtoto aliyekuwa amekufa yesu alipomuona akasema amelala.
8) Kumfanisha petro kupata samaki wengi aliyekuwa amevua samaki usiku kucha bila kupata au mafanio.
9) Viwete na Vipofu wa tangu kuzaliwa kutembea.au kuona kwa uweza wa mungu.
10) Kunyauka kwa mtini kwa neno la kinywa chaYesu

Mtumishi wa Yesu kama unamfuata Yesu hiyo ndiyo miujiza unaweza kujifunza kuweka msingi kwa kuanza ipo miujiza mingine imeachwa kama homework mfano kuambia mlima ngoka ukatupwe baharini ,mawe kupaza sauti na kumtukuza mungu,hayo yangelitendeka.

## 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**


Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 9332

**MWENGE— DAR-ES-SALAAM TANZANIA**



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034